**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Tisa - Tarehe 13 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE DR. FESTUS B. LIMBU):**

Hati ya Nyongeza ya Matumizi Na. 1 ya Mwaka 2003/2004 *(Supplementary Estimates of Expenditure No. 1 of 2003/2004).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 105

**Wabunge Wanachama wa SADC na ACP**

**MHE. PARSEKO V. KONE (k.n.y. MHE. DR. BATILDA S. BURIAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliochaguliwa kuliwakilisha Bunge kwenye Mabunge ya *SADC* na *ACP:-*

Je, ni nini wajibu/majukumu ya Wabunge hao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bunge la *SADC* au *SADC Parliamentary Forum* ni chombo kilichoanzishwa kutokana na Mkataba wa *SADC (SADC Treaty)* Ibara ya 9(2). Kwa sasa *SADC Parliamentary Forum* haina hadhi kamili ya Bunge, japo iko kwenye taratibu za kujibadilisha kuwa Bunge la *SADC,* kufuatana na mabadiliko yanayotokea ambapo katika Mkataba wa *African Union* (Jumuiya ya Afrika), inapendekezwa kuwepo kwa Mabunge ya Kanda kama ilivyo kwa Bunge la Afrika Mashariki na Bunge la *ECOWAS* kule Afrika Magharibi.

Mheshimiwa Spika, *SADC Parliamentary Forum* inaundwa na wawakilishi kutoka Mabunge wanachama wa nchi 12 za *SADC* ambazo ni Tanzania, Malawi, Zambia, Msumbiji, Lesotho, Swaziland, Botswana, Namibia, Afrika Kusini, Mauritius, Zimbabwe na Angola.

Mheshimiwa Spika, hakuna Bunge la *ACP* yaani *African Caribbean and Pacific Countries* bali kuna chombo kinachofanana na Bunge yaani *Joint Parliamentary Assembly* ambapo wanachama wake wanatokana na mwakilishi mmoja kutoka kila nchi za *ACP* ambazo kwa sasa ziko 81 wakiungana na Wabunge wanaowakilisha Bunge la Jumuiya ya Ulaya *(European Parliamentary).* Jina kamili ni *ACP-EU Joint Assembly.* Chimbuko la *ACP-EU Joint Assembly* ni Mkataba wa Lome uliowekwa saini mwaka 1975 na kuanzia mwaka 2000 unajulikana kuwa Mkataba wa Cotonou.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wabunge wa *SADC Parliamentary Forum* ni kuwakilisha nchi zao katika shughuli zote kama inavyotamkwa na Katiba ya chombo hicho. Majukumu hayo ni kujadili Mikataba na shughuli zote zinazofanywa na *SADC* kupitia Serikali za nchi wanachama na kutoa mapendekezo kwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za *SADC* kupitia Baraza lao la Mawaziri *(Council of Ministers).*

Mheshimiwa Spika, *SADC Parliamentary Forum* pia ina jukumu la kujenga mahusaino mbalimbali katika Kanda, kupitia Kamati zake za kudumu kama vile, Kamati ya Mahusiano ya Kikanda *(Inter-Regional Co-operation Committee),* Kamati ya Mahusiano ya Mabunge *(Inter Parliamentary Co-operation Committee)* na Kamati ya Mahusiano ya Jinsia na Kamati ya Kupambana na Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, *SADC Parliamentary Forum* pia ina jukumu la kuhakikisha chaguzi mbalimbali katika nchi wanachama zinafanyika kwa haki na uhuru ili kuendeleza na kulinda demokrasia na utawala bora. Katika kutekeleza jukumu hili *SADC Parliamentary Forum* inashiriki chaguzi hizo kama Mwangalizi wa Kimataifa. Kwa kushirikiana na Tume za Taifa za Uchaguzi za nchi za *SADC,* imeandaa *Norms and Standards for Elections in the SADC Region* na taarifa yake itawasilishwa Bungeni. Jukumu lingine ni kusimamia mipango inayotokana na Mikataba mbalimbali inayoridhiwa na nchi wanachama kama vile kuhusu masuala ya Ukimwi, kuondoa umaskini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, jukumu letu katika chombo cha *ACP-EU* ni kujadili masuala yanayohusu mahusiano yanayotokana na Mkataba wa Lome - Cotonou, utawala bora uwajibikaji na misaada mbalimbali inayotolewa na nchi za Jumuiya ya Ulaya kwenda kwa nchi za *ACP.* Jukumu lingine ni kujadili matatizo yanayotokana na utekezaji wa mipango iliyokubalika na kutengewa fedha na kupendekezwa njia na mikakati itakayosaidia kuondoa urasimu *(bureaucracy)* katika utoaji wa misaada hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Wabunge wa *ACP-EU* wanasimamia maslahi ya nchi wanazoziwakilisha kama Wabunge wa *EU* wanavyosimamia maslahi ya nchi za *EU* ambazo ndizo zinazotoa misaada. Mapendekezo yote ya Bunge la *ACP-EU* yanapitia kwenye Baraza la Mawaziri kwenda *European Commission* na Wakuu wa Nchi zote za *ACP* kwa utekelezaji.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kwamba ameeleza kwamba itabidi wanaowakilisha Bunge hili kwenye makundi hayo mbalimbali lazima walete taarifa Bungeni. Je, ni mara ngapi wameleta taarifa hiyo tukaijadili hapa Bungeni na kama hawakuleta si vema wawe wanaleta kama Kamati zinavyoleta taarifa zao tukajadili Bungeni? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hawa wawakilishi wetu taarifa zao zinapitia kwenye Kamati kama vile taarifa za wenzetu Wabunge wa Afrika Mashariki. Sasa inawezekana wenzetu wa Kamati wanajua zaidi lakini kwa utaratibu tuliojiwekea humu Kamati zetu zinawasilishwa mara moja kwa mwaka na mnajua mwaka mzima tulikuwa hatujapewa taarifa hata za Kamati za Kudumu na ndiyo maana sasa kuanzia wiki ijayo Mheshimiwa Spika ameweka utaratibu ambao utawezesha kuwasilisha taarifa hizi zote.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini ningependa kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wawakilishi hao wanawakilisha Bunge letu pamoja na maslahi ya nchi yetu na kwa kuwa kanuni zetu hazitoi nafasi kwa wawakilishi wetu kutoa taarifa rasmi Bungeni na kwa kuwa wenzetu wa nchi nyingine wanajadili na hilo ndilo tatizo tulilopata kwenye mikutano hiyo ya *SADC* na hata *ACP*.

Je, ni lini sasa kanuni zetu zitarekebishwa ili tuendane na tuwe sawa na nchi za wenzetu ambapo taarifa zinajadiliwa na zinarudishwa kwenye Mabunge hayo ili yaendane sawa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa uzoefu wake maana yeye ni mmoja wa hao wanaotuwakilisha huko na jambo hili nafikiri ni jema, kwa hiyo, nitaliwasilisha kwa Mheshimiwa Spika ili tuweze kulijadili na kulitolea uamuzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo limeshafika kwa Mheshimiwa Spika. *(Kicheko)*

Na. 106

**Umri wa Mgombea Kiti cha Urais**

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa kazi na majukumu ya Mheshimiwa Rais ni mengi na mazito yenye misukosuko na mihangaiko mingi inayohitaji nguvu za kutosha kukabiliana na kazi hizo na kwa kuwa ni kutokana na ukweli huo kwamba haifai kukabidhi majukumu hayo kwa mtu ambaye tayari ni mzee yaani kuanzia miaka 70 na kuendelea na kwa kuwa tunao utaratibu wa Rais kukaa madarakani kwa kipindi kinachoweza kufikia miaka 10.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka kuweka kiwango cha umri wa mgombea kiti cha Urais kwa mara ya kwanza kisizidi miaka 60?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MOHAMED SEIF KHATIB):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba majukumu ya Rais wetu ni mengi, lakini kuwa yana uzito, misukosuko na mihangaiko ya majukumu hayo sina hakika nayo hasa kwa mantiki ya utendaji. Kwa mujibu wa Ibara ya 39(i)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mtu anayetaka kugombea nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatakiwa kuwa na miongoni mwa mambo mengine, awe ametimiza umri wa miaka arobaini.

Mheshimiwa Spika, Katiba haijaweka ukomo wa umri wa anayetaka kuwa mgombea Urais katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa kutambua kuwa Rais anayo majukumu mengi katika kuliongoza Taifa, kuna Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na wengine ambao wanamsaidia katika uongozi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, endapo zitakuwepo sababu za msingi za kukidhi matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali haitasita kuangalia maoni juu ya umri wa mgombea kiti cha Urais katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sasa hata hivyo ziko taratibu za kufuatwa za kikatiba endapo itaonekana Rais hamudu shughuli kwa sababu za kiafya.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa kutokana na hali ya sasa ya dunia ya sayansi na teknolojia na uzoefu uliokuwepo kwamba Marais wengi katika nchi nyingi zilizoendelea na zinazoendelea kwa sasa Marais wanakuwa na umri ambao si mkubwa sana ili wakabiliane na hali ya sayansi na teknolojia na kwa kuwa Katiba ambayo Mheshimiwa Waziri ameizungumzia sasa ipo katika kufikiriwa kubadilishwa.

Je, haoni kwamba itakuwa ni muda muafaka kutokana na mazingira yaliyopo na kwa sababu tunazungumzia Katiba sasa tuweze kubadilisha ili ioane na pendekezo langu? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa tumekuwa tunazungumza sana kwamba vijana ni Taifa la kesho na imekuwa vigumu kusema kwamba vijana ni Taifa la sasa, sasa usemi huu unaweza ukabadilishwa basi ikawa vijana ni Taifa la kesho asubuhi? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MOHAMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, mimi sina mamlaka ya kugeuza usemi huo kwa sababu sina mamlaka ya Kikatiba wala kisheria. Kwa hiyo, watu waseme wanavyotaka wenyewe, ni hiari yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umri wa uongozi nafikiri hakuna maelewano duniani kwamba Rais wa nchi awe na miaka mingapi, hakuna Katiba wala Mkataba wowote ule. Kwa hiyo, kila nchi itategemea masharti yake yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini labda tuangalie uzoefu wetu hapa nchini kwamba Hayati Mwalimu Julius Nyerere alizaliwa mwaka 1922, akawa Rais wa Tanganyika mwaka 1962, wakati alipopata Urais alikuwa na umri wa miaka 40, alipostaafu alikuwa na umri wa miaka 63. Rais Alli Hassan Mwinyi kazaliwa mwaka 1925, kapata Urais mwaka 1985, alipoapishwa kuwa Rais alikuwa na miaka 60 na alipostaafu alikuwa na miaka 70. Rais Benjamin Mkapa kazaliwa mwaka 1938, kapata Urais mwaka 1995, alipoapishwa kuwa Rais alikuwa na miaka 57 na atakapokuja kustaafu atakuwa na miaka 67. Kwa hiyo, hakuna vigezo maalum kwenye suala hili. Tunaweza tukawa na Rais kijana akawa na vituko au Rais mzee akawa na viroja. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, itategemea Chama cha Siasa kimweke Rais gani ili ashinde katika mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa. *(Makofi)*

Na. 107

**Ujenzi wa Soko la Ruaha**

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1994 aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro wakati huo Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, kwa sasa Mbunge wa Songea Mjini aliweka Jiwe la Msingi la Ujenzi wa Soko la Ruaha pamoja na kuwapimia wafanyabiashara maeneo ya kujenga vibanda vya biashara kuzunguka soko hilo na kwa kuwa Serikali iliahidi kujenga soko katikati lakini ujenzi huo bado haujaanza wala upimaji wa Mji huo mdogo haujafanyika.

Je, ni lini ujenzi wa soko utaanza ili wananchi waweze kupata huduma za uhakika, bora na salama?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Semanini Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba jiwe la msingi la ujenzi wa soko la Ruaha liliwekwa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro wakati huo Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama mwaka 1994. Kama hatua za mwanzo za ujenzi wa soko hilo, Idara ya Ardhi ilipima maeneo ya vibanda vya biashara ambavyo wafanyabiashara wenyewe walichangia gharama za upimaji.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa soko la Ruaha umeshindikana kuanza kutokana na kutokuwepo kwa mchoro wa Kijiji cha Ruaha. Ukosefu wa fedha za kugharamia uchoraji wa ramani hiyo ndiyo msingi wa kutotekelezwa kwa mradi huu.

Jumla ya shilingi 3,500,000 zinahitajika kwa madhumuni hayo. Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa itatenga fedha hizo katika Bajeti yake ya mwaka 2004/2005. Baada ya kukamilisha michoro hiyo, Halmashauri itaendeleza juhudi za kupata fedha za ujenzi wa soko hili. Ninamsihi Mheshimiwa Mbunge tusaidiane kufuatilia suala hili na Halmashauri yake ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinapatikana ili kuwezesha zoezi hilo kuendelea.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba ni kweli ni muda mrefu na watatenga fedha hizo na ameniomba nimsaidie pale nitakapokuwa nafuatilia.

Je, kwa sababu sasa tumebakiza miaka miwili kumaliza vipindi vyetu na kufagilia CCM, yuko tayari kuhakikisha kwamba tunafagilia pamoja, soko hilo linapimwa ili CCM iendelee? *(Kicheko)*

Pili, kwa kuwa milioni tatu haifai hata kutamkwa humu Bungeni, hivi ni kweli Halmashauri inakosa milioni tatu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida ningeweza tu kusema kwamba majibu anayo Mheshimiwa Christopher Wegga maana anatoka kwenye Halmashauri hiyo hiyo. Lakini la kuweza kuongezea hapa ni kwamba tujitahidi, ndiyo maana nimesema tusaidiane, Halmashauri hiyo ipo chini yake yeye mwenyewe, nina hakika mkiifagilia vizuri jambo hili mnaweza kabisa mkakamilisha kabla ya mwaka 2005. Milioni tatu na laki tano zinaonekana ni chache na mimi nakubaliana naye kweli ni chache na pengine hiyo inaonyesha kwamba inawezekana Halmashauri yako haijaweka sana umuhimu kwenye eneo hili na ndiyo maana wanaona kwamba pengine hakuna haja, lakini mimi nina hakika tukisaidiana tutawasukuma waone kwamba pengine upo umuhimu.

Na. 108

**Upungufu wa Wauguzi - Vituo vya Afya vya K'harumwa na Nyang'hwale**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Vituo vya Afya vya K'harumwa na Nyang'hwale katika Jimbo la Uchaguzi Nyang'hwale vinakabiliwa na upungufu mkubwa wa wauguzi na pia vipo mbali na hospitali ya Wilaya iliyopo Mjini Geita kwa zaidi ya kilomita 100 na kwa kuwa wagonjwa wengi wakiwemo akina mama wajawazito wanapoteza maisha yao kwa kukosa usafiri wa kuwapeleka kwenye hospitali ya Wilaya kwa matibabu zaidi kutoka kwenye vituo hivyo vya Afya.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia vituo hivyo usafiri wa uhakika ili kunusuru maisha ya wagonjwa hususan akina mama wajawazito?

(b) Je, ni lini Serikali itavipatia vituo hivyo waganga na wauguzi wa kutosha pamoja na mtaalam wa Maabara?

(c) Je, ni nini hatma ya gari la wagonjwa lililokuwa katika Kituo cha Afya cha Nyang'hwale hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990 ambalo lilichukuliwa na Serikali kwa ajili ya matengenezo lakini halijarudishwa hadi leo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Nyang'hwale vipo vituo viwili vya Afya vya Nyang'hwale ambacho kipo umbali wa kilomita 68 kupitia Kasamwa na Kituo cha Afya cha K'harumwa ambacho kipo umbali wa kilomita 118 kupitia *Kahama Mine* kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Ili kuboresha huduma kwa wananchi wakiwemo watoto na akina mama wajawazito, Serikali bado inaendelea na juhudi za kupata magari ya kubebea wagonjwa kwa ajili ya Hospitali za Wilaya na Vituo vya Afya hasa vilivyo mbali ili kutatua tatizo sugu la magari ya wagonjwa.

Aidha, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Geita imepanga kuweka *Radio Call* katika Kituo cha Afya cha Nyang'hwale kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano kati ya Kituo hicho na Hospitali ya Wilaya. Kituo cha Afya cha K'harumwa kimewekewa jenereta ya umeme yenye uwezo wa *KVA 50* iliyonunuliwa na Halmashauri na majengo ya upasuaji na nyumba ya Daktari yanaendelea kujengwa.

(b) Mheshimiwa Spika, jitihada inafanywa ili kupata wataalam wa fani mbalimbali wanaohitajika katika Vituo vya Afya vya K'harumwa na Nyang'hwale. Kulingana na ikama ya Halmashauri vituo hivi vina upungufu wa wataalam kama ifuatavyo:-

- Vituo vyote havina Daktari bali kwa sasa vinaongozwa na Tabibu *(Clinical Officers)* ambapo kuna Tabibu mmoja kati ya watatu wanaohitajika kuwepo kwenye kila kituo.

- Kila kituo kina Wauguzi wawili kati ya Wauguzi tisa wanaohitajika. Kituo cha Afya K'harumwa kina Msaidizi maabara mmoja.

- Vituo vyote viwili havina *Dental Therapist* ambapo kila kituo kinahitaji kuwa na mtaalam mmoja wa meno.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 Halmashauri ilipata kibali cha kuajiri watumishi wa afya 21 na ikafanya idadi ya wataalam wa afya Kiwilaya kuwa 108. Aidha, kibali kimeombwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kujaza nafasi wazi zilizopo Wilayani kwa mwaka 2004/2005, ikiwa ni pamoja na Vituo vya Afya vya K'harumwa na Nyang'hwale. Aidha, Serikali itaendelea kutoa vibali vya ajira kulingana na uwezo unaokuwepo kifedha.

(c) Mheshimiwa Spika, gari namba *STG 5853* lililokuwa la Kituo cha Afya cha Nyang'hwale pamoja na magari mengine machakavu yalifutwa na Kamati ya Ufutaji Mashine na Mitambo *(KUMM)* na kuuzwa kwa kufuata taratibu za Serikali.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza kama ifuatavyo.

Moja, kwa kuwa ili kutatua matatizo ya elimu ya msingi Serikali ilibuni mpango wa *MMEM* yaani Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi na kwa kuwa masuala ya afya yanafanana na yale yale ya elimu ya msingi. Je, Serikali ipo tayari kuleta mpango au kubuni mpango wa *MMAM* yaani Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi ili kupata pesa za kujenga nyumba za Waganga Vijijini pamoja na ajira za watendaji wa kutosha? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa Serikali ina utaratibu wa kuwabadilishia Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Makatibu na Ma-*DC* magari mapya na kwa kuwa yale ya zamani sasa yanapelekwa kwenye idara mbalimbali. Je, Serikali itakuwa tayari sasa magari hayo baada ya kuachwa kwenye Idara za Serikali Wizarani au kwa Ma-*DAS* kuyapeleka kwenye Vituo vya Afya awamu kwa awamu ili kutatua tatizo la usafiri kwa Vituo vya Afya nchini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, inawezekana tu pengine katika kueleza jambo hili halielezwi kwa namna ambayo ingesaidia, lakini Serikali inao mpango tayari ambao unashughulikia sekta ya afya hasa kupitia *Basket Fund* ambapo ndiyo tunajitahidi kujaribu kuboresha mazingira katika Vituo na Zahanati zetu lakini vile vile katika hospitali za Wilaya.

Sasa kama lengo ni kuwa na kitu mahsusi kinaitwa *MMAM,* mimi nadhani la kutazama ni kuwa ni lazima tutumie maneno hayo au mengine, lakini utaratibu na mpango kwa kweli upo na unaendelea kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, suala la magari, tatizo ni fedha, kama fedha zingekuwepo suala hili la magari tusingekuwa tunalizungumza kwa namna tunavyolizungumza. Kwa hiyo, kwa sasa kuweka utaratibu wa kubadilisha magari kwa vituo zaidi ya 3,000 wakati fedha yenyewe ya kununua magari kukidhi vituo hivyo hazipo inakuwa kwa kweli ni kuanza *debate* nyingine kabla hujamaliza *debate* ya kwanza.

Kwa hiyo, mimi nadhani tufanye subira, Serikali inajitahidi sana kutatua tatizo hili ingawa tunajua kabisa halitakuwa pengine la kudumu, lakini angalau kwa muda tunaamini Serikali imeshasikiliza hoja hii na inaifanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Waziri amekubali kwamba pangekuwa na fedha vituo vya Afya vingepata magari. Sasa kwa vile kuna vituo vya afya vyenye magari lakini yamerudishwa Wilayani kutokana na Waraka wa Serikali kwamba magari yote yawe *pool* kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Je, Waziri atakubali magari hayo ya Vituo vya Afya yarudishwe kwenye vituo hivyo na hasa Kituo cha Afya Maberera kilicho kilomita 120 kutoka Hospitali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, magari yanarudishwa Wilayani si kwa sababu kuna Waraka ambao unayataka magari haya yarudi Wilayani. Magari yanarejeshwa Wilayani kwa sababu mengi ni mabovu, uwezo wa kutengenezwa katika Vituo vyetu vya Afya haupo ndiyo maana Serikali kwa kutumia Halmashauri zetu imekuwa inayarejesha pale, wanajitahidi kuyatengeneza, yale yanayopata unafuu kidogo ndiyo hayo ambayo yanabakizwa Wilayani ili yaweze kufanya safari kulingana na mahitaji ya vituo ambavyo viko *scattered.* Nadhani haya ndiyo maelezo ya msingi ambayo pengine Serikali inaweza ikayatoa kuhusiana na jambo hilo.

Na. 109

**Dhana ya Miradi Endelevu**

**MHE. PHILLIP A. MAGANI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kubuni na kutayarisha miradi ya maendeleo endelevu Tanzania yaani miradi ambayo baada ya kutekeleza awamu ya kwanza miradi hiyo inajiwekea akiba ya fedha ili baadaye ikipevuka iweze kujilipia gharama zake ikiwa ni pamoja na gharama za upanuzi na kwa kuwa dhana hiyo inahusu miradi yote pamoja na miradi ambayo hugharamiwa kwa ubia na wahisani:-

(a) Je, ni miradi mingapi na ipi ya aina hiyo ambayo imeanzishwa kwa dhana endelevu tangu mwaka 1995?

(b) Je, ni sababu zipi za kimsingi zilizosababisha mradi kama ule wa *IFAD* wa kufadhili mikopo kwa wakulima wa mazao ya chakula kushindwa kujiendeleza mwishoni mwa kipindi cha mradi (miaka sita) baada ya wahisani kumaliza kipindi chao cha kusaidia kugharamia mradi huo?

(c) Je, ni kweli kuwa Serikali haiko makini katika kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo na ndiyo maana inashindwa kuwa endelevu pamoja na dhana mpya iliyoongezwa yaani dhana shirikishi na Serikali inachukua hatua zipi za dhati ili kuhakikisha kwamba hali ya miradi kushindwa kuwa endelevu haitokei tena na hasa miradi inayosaidiwa na wahisani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya kubuni na kutayarisha mipango ya maendeleo endelevu Tanzania hususan katika sekta ya umma inazingatia misingi shirikishi ya wadau wote ambao hushirikishwa kikamilifu katika kubuni, kuchagua, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathmini mipango na miradi ya maendeleo. Dhana hii inatoa kipaumbele katika kuweka mazingira muafaka ya kudumisha maendeleo na kujenga uwezo wa wadau ili washiriki kikamilifu katika uendelevu wa miradi hiyo hasa baada ya kupevuka. Hii ni kwa kwa sababu miradi mingi ya sekta ya umma ina lengo kubwa la kutoa huduma kwa wananchi ili kukuza ustawi wa jamii na uchumi jumla. Hivyo dhana shirikishi ndiyo inatumika kujenga uwezo wa walengwa kuendesha miradi hiyo wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine miradi mingi inayojiwekea akiba ya fedha ili baadaye ikipevuka iweze kujilipia gharama zake yenyewe ikiwa ni pamoja na gharama za upanuzi ni ile inayobuniwa na sekta binafsi ambayo lengo lake kubwa ni kupata faida.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Phillip Magani, Mbunge wa Ruangwa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna miradi mingi hapa nchini inayotekelezwa na Wizara, Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya mbalimbali ambayo imeanzishwa tangu mwaka 1995 kwa dhana ya maendeleo endelevu. Mfano wa miradi hiyo ni kama hii ifuatayo:-

(i) Mradi Shirikishi wa Jamii wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji unaotekelezwa katika Wilaya 12 za Babati, Dodoma Vijijini, Igunga, Iramba, Kwimba, Mbulu, Manyoni, Maswa, Mpwapwa, Nzega, Shinyanga na Misungwi kuanzia mwaka 2000.

(ii) Mradi wa Kuendeleza Mabonde na Kuboresha Kilimo cha Umwagiliaji ambao unatekelezwa katika mabonde ya Mito ya Pangani na Rufiji tangu mwaka 1996.

(iii) Mradi wa Kusaidia Maendeleo ya Kilimo Wilayani unatekelezwa katika Mikoa ya Iringa na Mbeya kuanzia mwaka 2003.

(iv) Mradi wa Kuendeleza Mfumo wa Masoko ya Mazao ya Kilimo unatekelezwa katika Wilaya 36 za Nyanda za Kaskazini na Juu Kusini kwenye Mikoa ya Tanga,Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma kuanzia mwaka 2003.

(v) Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji unatekelezwa katika Wilaya 28 zikiwemo Wilaya nane ambazo zimeshaanza utekelezaji ambazo ni Morogoro, Nachingwea, Masasi, Iringa, Hanang, Arumeru, Hai na Singida.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa *IFAD* wa kufadhili mikopo kwa wakulima wa mazao ya chakula katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ulifanikiwa sana na ukawa kiini cha kuanzishwa kwa utekelezaji wa Mradi wa *Rural Financial Services* kwenye Mikoa hiyo.

Mradi huo unaendelea kufadhiliwa na *IFAD* na umejikita zaidi kwenye dhana ya maendeleo endelevu. Hivyo si kweli kuwa mradi wa *IFAD* ulishindwa kujiendeleza baada ya wahisani kumaliza kipindi chao.

(c) Mheshimiwa Spika, siyo kweli kuwa Serikali haiko makini katika kutayarisha na kusimamia miradi yake. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali iko makini katika kutayarisha na kusimamia mipango na miradi ya maendeleo endelevu ndiyo maana inaendelea kuimarisha dhana mpya ya kupanga mipango na miradi kwa kutumia mbinu shirikishi ya wadau wote.

Ili kudumisha azma hii, hatua zinazoendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa miradi yote inayotekelezwa na Serikali na kufadhiliwa na Wahisani inaendelea kuwa endelevu ni pamoja na kuhakikisha kuwa mbinu hizi shirikishi zinaanzia katika ngazi za Vijiji na miradi inamilikiwa na wananchi wenyewe pamoja na kuzingatia uendelezaji wa raslimali watu, jinsia na utawala bora katika matumizi ya raslimali.

Na. 110

**Bwawa la Kalimawe**

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA** aliuliza: -

Kwa kuwa bwawa la Kalimawe lenye ukubwa wa mzunguko wa kilomita za mraba 32 lilichimbwa mwaka 1959 katika Kata ya Ndungu Kijiji cha Kalimawe Wilayani Same; na kwa kuwa tangu bwawa hilo lichimbwe hadi sasa limekuwa likipokea maji ya mito ya Hingilili na Yongoma ambayo mara nyingi yanakuwa na mchanga na matope ambayo yamelijaza bwawa hilo na kupoteza ubora wake na kuashiria kutoweka:-

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo?

(b) Je, Serikali inaweza kuwaahidi wananchi wa Kata za Ndungu, Kihuria, Bandera, Gonja, Mamba Miamba na kadhalika, ambao karibu asilimia 80 ya wakazi wa Kata hizo wanategemea uvuvi wa samaki kutoka katika bwawa hilo na kwamba itawasaidia kuondoa matope na mchanga uliojaa kwenye bwawa hilo ili wananchi waendelee na shughuli zao za uvuvi?

(c) Kwa kuwa maji kutoka kwenye mradi wa umwagiliaji wa mpunga wa Ndungu huwa na dawa na mbolea za chumvichumvi kutoka mashambani; je maji haya hayawezi kuwaathiri samaki na mayai yao kwenye bwawa hilo?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo la kujaa mchanga na tope katika bwawa la Kalimawe na matokeo yake ni kupoteza ubora wa bwawa hilo. Matatizo haya yanatokana na kutozingatia kanuni za utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla. Upo uharibifu unaofanywa na wananchi wanaoishi jirani na mito ya Hingilili na Yongoma kwa kilimo kando kando ya mito hiyo, ukataji wa miti na uoto wa asili kando kando ya bwawa na mto.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kushirikiana na wananchi wa Kata za Ndungu, Kihuria, Bandera, Gonja na Mamba Miamba katika utekelezaji wa mipango yao ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuondoa matope katika bwawa la Kalimawe tukiombwa kufanya hivyo na wananchi wenyewe wakitimiza wajibu wao kama ulivyofafanuliwa katika Sera ya Maji.

(c) Serikali haina taarifa za kuathirika kwa samaki na mayai yao kutokana na mbolea za chumvi chumvi za kilimo zinazotumika katika mradi wa umwagiliaji wa mpunga uliopo Ndungu. Hata hivyo, Serikali inaahidi kufuatilia suala hili kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara yangu ili kuainisha kiasi cha uchafuzi wa maji na athari kwa viumbe wanaoishi kwenye bwawa hilo.

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ni hodari sana wa kutembelea Mikoa na kujionea mwenyewe matatizo yanayohusu Wizara yake; na kwa kuwa nina uhakika kuwa siku za karibuni Mheshimiwa Waziri hajatembelea Wilaya ya Same na Kata ya Ndungu kujionea ni jinsi gani tatizo hili ni kubwa sana kwa wananchi wa Kata husika. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akawaambia nini wananchi hawa hasa akijua kwamba wanaathirika kwa upande wa kilimo na kitoweo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufikiria eneo la Same ambako ndiko anakotoka, nampongeza sana kwa uamuzi huo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninakubali pendekezo la kufuatilia suala hilo na nikipata nafasi wakati muafaka tutakwenda Same na wataalamu wanaohusika. *(Makofi)*

Na. 111

**Miradi ya Maji Vijiji vya Ng'wamakalanga na Ng'wang'osha**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (k.n.y. MHE. ROBERT J. BUZUKA)** aliuliza :-

Kwa kuwa miradi ya maji katika vijiji vya Ng'wamakalanga na Ng'wang'osha iliyoanzishwa katika miaka ya 1970 imeharibika na kusababisha matatizo makubwa ya maji katika eneo hilo na vijiji jirani hasa ikizingatiwa kuwa malambo yaliyokuwapo yamejaa tope: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuifufua miradi hiyo ili kuondoa tatizo la maji na kuepusha maradhi yanayowakumbuka wananchi kutokana na utumiaji wa maji yasiyo salama?

(b) Kwa kuwa Vijiji vya Sayu, Shillabela na Mg'wasingu vilikuwa vinahudumiwa na malambo ambayo sasa yamejaa tope na hukauka mapema; je, ni lini Serikali itasaidia nguvu za wananchi katika kuchimba upya malambo hayo ili yaweze kuhifadhi maji kwa kipindi chote cha kiangazi?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Robert Jacob Buzuka, Mbunge wa Solwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo: -

Vijiji vya Ng'wamakalanga na Ng'wang'osha na Nyamalongo kwa pamoja vilikuwa vinahudumiwa na chanzo cha maji ya bwawa la Mwantini. Mradi huu ulifanya kazi kuanzia miaka ya 1970 hadi 1987 uliposimama kutokana na kuibiwa kwa mashine kusukuma maji.

Kwa mara ya kwanza mashine hiyo iliibiwa mwaka 1988 lakini ilipatikana kwa ushirikiano wa Polisi na wananchi na mtuhumiwa kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Baadaye tena mwaka 1989 iliibiwa ikiwa mikononi mwa Serikali ya Kijiji cha Ng'wang'osha na haijapatikana hadi leo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

(a) Kwa upande wa vijiji vya Sanyu, Shillabela na Ng'wasiga, Serikali kwa kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Mkoani Shinyanga, inahamasisha wananchi kuchangia fedha kidogo ili kupata fedha zingine kutoka kwenye Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa malambo.

Hadi sasa, wananchi bado hawajakamilisha michango yao, lakini fedha kutoka kwenye programu zipo tayari na zinasubiri wananchi watimize wajibu wao ili ujenzi uweze kuanza. Kijiji cha Ng'wasingu kimekamilisha ujenzi wa bwawa jipya kwa kushirikiana na Shirika la *World Vision International* ambao nachukua nafasi hii kuwashukuru sana.

(b) Serikali ina mpango wa kufufua mradi wa maji wa bwawa la Mwantini chini ya Mpango wa usambazaji maji vijijini katika Mkoa wa Shinyanga unaogharamiwa na msaada kutoka Serikali ya Uholanzi. Hadi sasa hivi jumla ya shilingi milioni 6 zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa bwawa. Fedha zaidi za ukarabati wa mradi zitapatikana baada ya wananchi kuchangia na kuwasilisha maombi yao kwenye Halmashauri ya Wilaya. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na uongozi wa Wilaya kuwahamasisha wananchi ili wachangie mradi huu. *(Makofi)*

Na. 112

**Mfuko wa Pembejeo**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imeamua kuanzisha Mfuko wa Pembejeo kwa lengo la kutoa mikopo kwa wakulima; na kwa kufanya hivyo kunainua hali ya kilimo nchini:-

(a) Je, kila Mkoa utapata mikopo hiyo au itakuwa ni kwa baadhi ya Mikoa tu?

(b) Je, Mkoa wa Shinyanga umepangiwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilianzisha Mfuko wa Pembejeo kwa Sheria Na. 9 ya mwaka 1994, kwa lengo la kuwawezesha wanafanyabiashara *(stockists)* kuagiza na kusambaza pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima nchini.

Kwa hiyo, wafanyabiashara wa pembejeo kwenye Mikoa yote wana haki sawa ya kupata mikopo kutoka kwenye mfuko huo, ilimradi maombi ya mikopo hiyo yatimize masharti na vigezo vilivyowekwa.

(b) Tangu Mfuko huo ulipoanzishwa mwaka wa 1994 hadi mwezi wa Desemba, 2003, mikopo ya shilingi 485,198,000/= ilikuwa imetolewa kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Shinyanga. Aidha, hadi tarehe 15 Januari, 2004 Mkoa wa Shinyanga ulikuwa umewasilisha maombi mapya sita ya mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 70 kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo na maombi 34, yenye thamani ya shilingi 110,106,000/= kwa ajili ya kukarabati matrekta. Maombi hayo yanaendelea kushughulikiwa.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mpango huu hata mwaka 1994 uliweza ukatolewa na Serikali, lakini utoaji huo haukuwa wa kuridhisha kwa sababu uliishia kwa watu wachache wajanja ambao hawakuweza kuwafikishia walengwa. Je, kwa sasa hivi mkakati utakuwaje wa kuweza kuwafikishia walengwa ambao wanatakiwa wapate mikopo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA :** Mheshimiwa Spika, mikopo yote inaanza Wilayani Meatu, anayetaka kukopa iwe mwananchi au *stockists* anapitisha maombi kupitia Afisa Kilimo na *DED* ndiyo anatoa *recommendation,* ndipo inafika kwa Mkurugenzi wa Mfuko wa Pembejeo. Ikifanyika hivyo na Mheshimiwa Mbunge akifuatilia tuna hakika ujanja ujanja huu utakoma. *(Kicheko)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa bei za pembejeo kama mbolea ni kubwa sana na kuna tetesi kwamba huko nje bei za pembejeo hizo ni rahisi. Je, Serikali inachukua hatua gani ya kufuatilia hizo bei huko nje kama ni sahihi wanavyotuletea wafanya biashara hapa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, sina uhakika kama pembejeo ni rahisi kiasi hicho. Sisi tungependa sana haya mambo rahisi yafike kwa wananchi wetu. Naomba tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi cha maswali na majibu anieleze ni wapi huko tutazitafuta huko huko. *(Kicheko)*

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja ndogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Serikali ilishawahi kutoa mikopo ya namna hii kipindi kilichopita na wafanya biashara wakawa wameitumia mikopo hiyo kinyume na ilivyokusudiwa. Je, Serikali imechukua hatua gani dhidi ya wahusika ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinarudi na kufanya kazi iliyokusudiwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli ilitokea hivyo na tulifuatilia kisheria tukakuta kulikuwepo na udanganyifu mwingi tu, wengine waliweka vitu vyao rehani kumbe vilikuwa si hivyo ilivyokuwa, tumebadilisha sasa.

Kwanza, tumefuatilia na masuala mengine yako Mahakamani ya wahusika. Lakini sasa utaratibu ni kuwa kwanza itabidi walete *pro-forma invoice* ya hicho kitu unachoomba, halafu maombi yote yanapitishwa Benki. Sasa sisi tukiwa makini katika Wizara na benki zikiwa makini kwa uchungu wa fedha zake naamini mambo sasa ni bora zaidi kuliko ilivyokuwa wakati huo. Naomba Mheshimiwa Mbunge aamini hivyo.

Na. 113

**Matumizi ya Maji ya Mvua**

**MHE. LEONARD M. SHANGO** aliuliza:-

Kwa kuwa majanga ya njaa yaliyolikumba Taifa letu kwa kiwango kikubwa yanasababishwa na ukame na pia kuwa na sera mbovu za kilimo ambayo haizingatii kwa matendo umuhimu wa kilimo bora cha umwagiliaji ambapo uvunaji maji ya mvua kama mabwawa pamoja na miundombinu yote inayotakiwa kufikisha maji mashambani:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kitendo cha kuendelea kuomba misaada wakati wa njaa ni kulidhalilisha Taifa na wananchi wake mbele ya nchi ambazo suala la njaa limepata ufumbuzi wa kudumu kwa kuwawezesha wakulima wake kujenga miundombinu ya uvunaji maji kwa matumizi ya kilimo cha kisasa cha umwagiliaji mashamba?

(b) Je, Serikali inasemaje na inajifunza nini kuhusu nchi ambazo zipo ndani ya kanda za majangwa ambapo suala la kunyesha mvua wakati wowote ni kitu kisichokuwa cha kawaida lakini kwa kutumia teknolojia ghali zaidi zinatumika kwa kilimo cha kisasa maji yaliyovunwa kutoka ardhini na kwa hiyo matukio ya njaa ya chakula ya mara kwa mara hayapo kabisa?

(c) Je, Serikali ina mipango gani kisera ya kulihakikishia Taifa kuwa tatizo la matukio ya njaa ya mara kwa mara litapata ufumbuzi wa kudumu na kulinusuru Taifa hili na aibu za omba omba, misaada ya chakula cha njaa kwa tatizo ambalo lingeepukika kama sio kujenga mitandao ya miundo mbinu ya mabwawa, mifereji, mabomba na pampu za kufikisha maji ya kumwagilia mashamba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Matatizo ya uvunaji wa maji kwa ajili ya kumwagilia mashambani hayatokani na ubovu wa sera. Tunazo sera nzuri sana. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 2000 inahimiza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani katika kuongeza uzalishaji wa mazao ili kufikia lengo la kujitosheleza kwa chakula. Sera ya kilimo ya mwaka wa 1997 na Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo wa mwaka wa 2001, navyo vinatilia suala hili msisitizo.

Tatizo kubwa la miradi ya umwagiliaji maji mashambani ni gharama kubwa sana zinazotakiwa kujenga miundombinu na gharama hizo huwa kubwa zaidi inapobidi kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua. Ili kupata manufaa makubwa kutokana na fedha kidogo zinazopatikana kila mwaka, miradi yenye gharama nafuu, inayohudumia maeneo makubwa na inayonufaisha wananchi wengi hupewa kipaumbele katika kutengewa raslimali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Leonard Shango, kwamba ni aibu kwa Tanzania kulazimika kuomba misaada ya chakula kutoka kwenye nchi au wahisani mbalimbali.

Hata hivyo, wakati huu ambapo tunatekeleza mipango itakayotuwezesha kujitegemea kwa chakula, tunapopata majanga ya njaa inatubidi tutafute chakula kwa kutumia fedha zetu na misaada yoyote tutakayoweza kupata. Wakati wa utawala wa ubaguzi wa rangi wa Afrika Kusini ambapo Tanzania iliupinga kwa hali na mali, Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Nyerere, aliwahi kusema kwamba kama wananchi wake wangekuwa katika hatari ya kufa kwa njaa, angekuwa tayari kutafuta misaada ya kuwanusuru kutoka Afrika ya Kusini. Hata leo Serikali ya CCM haitaacha Watanzania waathirike na njaa ili kuepuka aibu ya kuomba chakula na ni dhahiri kwamba kuathirika kwa wananchi ni aibu kubwa zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, wataalamu wetu wa umwagiliaji maji mashambani wametembelea nchi nyingi duniani kuhudhuria mafunzo ya taaluma na kujifunza kutokana na mbinu zinazotumiwa na nchi hizo. Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula alitembelea nchi ya Israel katika mwezi wa Septemba, 2003. Tatizo sio kutokujua ni nini cha kufanya bali ni uwezo wetu mdogo wa kuwekeza kwenye mipango ya umwagiliaji maji mashambani.

(c) Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu swali Na. 107 la Mheshimiwa Leonard Shango kwenye Mkutano wa 13 wa Bunge lako Tukufu, nilieleza hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa na Serikali kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

Napenda nirudie tena kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kadri hali ya kifedha itakavyokuwa inaruhusu Serikali itawekeza kwa wingi zaidi katika kutekeleza Mpango Kamambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Katika miaka iliyopita, Serikali ilijenga mabwawa 16 yenye ukubwa mbalimbali ambayo yanaendelea kutumika kwenye Mikoa ya Dodoma, Singida na Mara. Mwaka wa 2003/2004, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya ya ukarabati wa ujenzi wa mabwawa 11 katika Mikoa saba ya Tanzania Bara, ukiwemo Mkoa wa Singida. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi milioni 220 zimetengwa kwa ajili ya mabwawa ya Tyeme, Masagi na Kironda-Datali yaliyoko Mkoani Singida.

Aidha, programu Husishi ya Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani, itajenga jumla ya mabwawa madogo manane Mkoani Singida, kati ya hayo mabwawa matatu yako Wilayani Iramba. Serikali pia imejenga visima vifupi 36 katika Mikoa sita, vikiwemo visima vinne vya Mkoa wa Singida.

Pamoja na kupanua kilimo cha kumwagilia maji mashambani kama mbinu ya kujitosheleza kwa chakula, Mikoa na Wilaya zinazopata mvua za kuaminika kila mwaka, zimepatiwa mahitaji yake ya pembejeo na zana za kilimo ili kuziwezesha kuzalisha chakula kwa viwango vya juu iwezekanavyo.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wa Wilaya ya Iramba kwa kuwa sasa wameanza kupoteza maisha kutokana na njaa na Serikali ina mipango gani ya haraka ya ziada ili kusudi kuharakisha kupeleka chakula katika Wilaya ya Iramba kwa sababu kuna wananchi ambao wameathirika sana hasa kwenye kata za Ulungu, Mtekete, Kaselya, Shelui, Twike, Kidaru na Tulia? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula ikishirikiana na *Disaster Department* iliyoko katika Ofisi ya Waziri Mkuu, inachukua kila hatua iwezekanavyo kufikisha chakula kwa wananchi walioathirika na siyo Singida peke yake na Dodoma ni mojawapo, Shinyanga, Singida na kwingineko.

Kwanza, tunahamisha chakula cha ziada kilichopo kutoka Mkoa wa Rukwa na Ruvuma kukisogeza katika maeneo haya kwa ajili ya tahadhari. Aidha, wafanyabiashara wamehamasishwa kuagiza chakula kwa wingi.

Pili, nchi marafiki tumeomba msaada, hii ikiwa ni pamoja na nchi za jirani. Lakini vilevile Serikali imetenga fedha kushughulikia suala hili na siyo hivyo tu Kenya kama tulivyoelezwa hapo nyuma nadhani juzi juzi tu tumeagiza na kulipia tani 10,000 na tutaongeza.

Mheshimiwa Spika, aidha, mipango iko mbioni kuongeza chakula kwa sababu katika *Supplementary Estimate* zilizopo leo napo tunaomba Bunge lipitishe kuongeza uwezo kukabiliana na tatizo hili. Siyo tu Singida bali popote Tanzania, naomba mtusaidie.

Na. 114

**Ufugaji wa Samaki**

**MHE. GWASSA A. SESABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi hasa vijana wanaunda vikundi vidogo vidogo kwa ajili ya ufugaji wa samaki na wamechimba visima vingi kwenye pembe zote za Wilaya, na kwa kuwa Wilaya haina wataalamu wa Idara ya Maendeleo ya Samaki:-

(a) Je, ni lini Serikali itatuma wataalamu wa samaki kwenye maeneo ambako shughuli za ufugaji wa samaki zinafanyika kama Ngara na kwingineko ili kuongeza msukumo na ari ya kuifanya kazi hiyo ili vijana waweze kuondokana na umaskini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kutoa mafunzo na misaada ya vifaa kwa vikundi hivyo na vingine vitakavyojitokeza?

(c) Je, Waziri atakuwa tayari kutembelea Wilaya ya Ngara ili ajionee mwenyewe juhudi zinazofanywa na vijana katika zoezi zima la ufugaji wa samaki?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, naomba kutoa maelezo ya awali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Wilaya ya Ngara ni moja ya Wilaya chache nchini ambazo hazina watalaamu wa Sekta ya Uvuvi. Kutokana na tatizo la upungufu wa wataalamu hao, Wizara yangu imekuwa ikishirikisha wataalamu wa Sekta nyingine za Maliasili na zile za kilimo katika kuendeleza shughuli za uvuvi hususan ufugaji wa samaki kwenye maeneo yale ambayo hayana wataalamu wa Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara imetuma Wataalam wa Uvuvi kwenye maeneo ambako shughuli za ufugaji wa samaki zinafanyika Wilayani Ngara. Wataalamu hao wametembelea maeneo husika kuanzia tarehe 29 Januari, 2004 hadi 6 Februari, 2004 na kuwasilisha taarifa ya kitaalamu itakayotumiwa na Wizara yangu kuandaa utaratibu wa kuendeleza shughuli za uvuvi Wilayani Ngara.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inayo programu ya mafunzo ambayo chini yake mafunzo mbalimbali hutolewa kwa wadau wa sekta zote za Maliasili ikiwemo Uvuvi. Chini ya Programu hii umeandaliwa mpango wa utekelezaji wa mafunzo hayo ambayo hufanyika katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa upande wa Wilaya ya Ngara, mpango wa mafunzo ya kuhamasisha ufugaji bora wa samaki utatekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu sasa hivi haina mpango wa kutoa misaada ya vifaa kwa vikundi vya wafugaji samaki nchini. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge aiunge mkono Wizara katika kuwahamasisha wananchi juu ya kuomba mikopo kutoka kwenye Taasisi za fedha na hata kutoka kwenye Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Aidha, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, avihamasishe vikundi hivyo juu ya kuanzisha mifuko ya kuweka na kukopa ili waweze kuongeza mitaji yao kwa ajili ya uzalishaji.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa mara nyingine kuwa nitajitahidi kutafuta muda unaofaa wa kuitembelea Wilaya ya Ngara kujionea shughuli za kuendeleza Sekta ya Uvuvi Wilayani humo kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha 2003/2004.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kutia moyo. Lakini hata hivyo, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa msimamo wa Serikali sasa hivi katika kuondoa umaskini ni kuhakikisha kwamba Sekta Binafsi inasimamiwa na kuwezeshwa ili kuinua uchumi wa nchi; na kwa kuwa tunao vijana wengi ambao sasa wanamaliza masomo na wanamaliza mafunzo, lakini kwa ukosefu wa ajira hawana mahali pa kwenda isipokuwa kujiajiri wenyewe na maeneo kamili ya kuweza kujiajiri ni pamoja na ufugaji wa samaki. Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kwamba sasa umefika wakati wa kuwa na Vyuo vingi vya kutosha kufundisha wataalam kusudi kuweza kupelekwa katika Wilaya ambazo hazina wataalam kama hivi alivyotamka Wilaya ya Ngara ili kusudi vijana wetu waweze kuondokana na matatizo ya kuingia katika vitendo viovu kwa sababu hawana ajira?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba kuna umuhimu sana wa kuwawezesha vijana wetu katika sekta hii ya uvuvi. Lakini kama nilivyokuwa najibu swali la msingi ni kwamba tutatilia mkazo juu ya mafunzo. Sasa mafunzo yanawezekana na pengine yatakuwa muhimu ya pale kwa pale. Mafunzo kwa mfano ya utengenezaji boti, mafunzo ya uvuvi, mafunzo ya kutumia nyenzo za kisasa na kadhalika. Kwa hiyo, mafunzo ambayo kwa kweli tutasisitiza ni mafunzo ambayo yatatolewa pale kwa pale katika maeneo yetu. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tuna mabwawa mengi sana katika Wilaya ya Kiteto na tulipandikiza samaki na hao samaki sasa wamekuwa wakubwa na wanawapa taabu sana ng'ombe wakati wakinywa maji.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ingekuwa vizuri kwa Wizara kutupelekea Afisa Uvuvi ili aweze sasa kutuelekeza namna ya kufuga hawa samaki na kusababisha na sisi kuanza kujifunza kula samaki? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nafurahi sana kwamba Mheshimiwa Benedict Losurutia, anatilia mkazo juu ya ulaji wa samaki.

Napenda kusisitiza kwa Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wote kwamba, kwa kweli samaki ndiye ambaye ana protini zaidi kuliko nyama nyingine na umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini ninapenda kusema kwamba pale ambapo tumekuwa na mabwawa ya samaki wakati huo huo wananchi huwa wanafundishwa jinsi ya kuvua hao samaki. Kwa hiyo, hilo tutalifuatilia. *(Makofi)*

Na. 115

**Uvuvi Katika Ziwa Nyasa**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa inafahamika kuwa Ziwa Nyasa halina Samaki wengi kama maziwa mengine hapa nchini:-

Je, katika hali ya namna hii Serikali itawasaidia kwa njia gani wavuvi wa Ziwa hilo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kueleza katika Bunge lako Tukufu wakati nikijibu swali Na. 57, katika Kikao cha Nane cha Mkutano wa Bunge, Ziwa Nyasa halina samaki wengi ukilinganisha na maziwa mengine kwa kuwa sehemu kubwa ya maji ya Ziwa hilo iko kwenye kina kirefu cha maji zaidi ya mita 250 ambacho kisayansi hakina Samaki wengi kutokana na uchache wa hewa safi aina ya oksijeni.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha Samaki walioko Ziwa Nyasa ni tani 168,400. Samaki wanaoweza kuvuliwa bila kuathiri vizazi vijavyo vya samaki ni tani 33,300.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba, wavuvi wa Ziwa Nyasa wanavua wastani wa tani 20,000 za samaki kwa mwaka, Serikali imechukua hatua za makusudi zitakazowawezesha wavuvi kuongeza mavuno ya samaki kufikia kiwango cha wastani wa tani 33,300 kwa mwaka. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kufanya tathmini ya hali halisi ya sekta ya uvuvi kupitia Mpango Kamambe wa Kuendeleza Uvuvi. Mpango huo ulikamilika Mei, 2002 na umeainisha maeneo 15 ya kupewa kipaumbele. Kati ya maeneo hayo, Programu ya kuboresha vyombo vya Uvuvi Ziwa Nyasa imepewa kipaumbele. Programu hiyo inajumuisha teknolojia ya kisasa ya ujenzi wa maboti ya uvuvi. Upatikanaji wa vyombo vya kisasa vya uvuvi utawezesha wavuvi kuongeza kiwango cha samaki wanaoweza kuvuliwa bila kuathiri vizazi vijavyo kutoka tani 20,000 hadi tani 30,300. Ili wananchi waweze kupata boti hizo, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya kujenga uwezo na kuwahamasisha kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali ili waweze kuomba mikopo kutoka vyombo vya fedha.

Pia Wizara itaendelea kuwahamasisha wananchi kuunda mifuko ya kuweka na kukopa kwa lengo la kununua zana bora za uvuvi na hivyo kuongeza mavuno ya samaki. Ongezeko la mavuno ya samaki litainua kipato kwa wavuvi na chakula kwa wananchi.

(ii) Kuwahamasisha na kuwapatia wananchi mafunzo ya ufugaji samaki ili wajihusishe katika kufuga samaki kwa lengo la kuongeza kipato. Jumla ya wananchi 740 wa Wilaya za Namtumbo, Songea na Mbinga wamenufaika na mafunzo hayo katika mwaka huu wa fedha.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa Serikali ina mpango kamambe ama mpango maalum kwa ajili ya kuboresha shughuli za uvuvi Ziwa Nyasa na programu hiyo hivi sasa bado haijaanza, je, programu hiyo itaanza lini? Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba programu hii ya *Master Plan* imeshaanza na ilimalizika mwaka 2002. Lakini kutokana na tathmini ambayo imefanyika ni kwamba sisi wenyewe pia tunashughulikia suala hili. Nilieleza maeneo yale ambayo kwa kweli tayari tumefanya mafunzo ya ufugaji wa Samaki kuzunguka ziwa hili la *Nyasa.*

Na. 116

**Athari za Wakimbizi Nchini**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imekumbwa na wimbi kubwa la Wakimbizi ambao wanakimbia vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Burundi na hivyo kuathiri mazingira na huduma mbalimbali za jamii katika Mikoa inayopakana na nchi hiyo tangu mwaka 1990:-

(a) Je, Tanzania imepata misaada kiasi gani kutoka kwenye Taasisi za Kimataifa na misaada hiyo imetumika katika maeneo gani yaliyoathirika na ni fedha kiasi gani kinatumika kwa kila eneo?

(b) Je, ni nchi gani rafiki zilizotoa misaada moja kwa moja kwa Tanzania?

(c) Je, Tanzania yenyewe imeingia gharama za namna gani na kiasi gani tangu Julai, 1995 hadi Juni, 2002?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na athari za kiusalama, kijamii na kiuchumi zinazotokana na nchi yetu kuhifadhi mamia ya maelfu ya Wakimbizi hususan katika Mikoa ya Kigoma na Kagera, Tanzania imekuwa ikipata misaada ya aina mbalimbali kutoka Jumuiya ya Kimataifa kupitia Taasisi mbalimbali za Kimataifa. Misaada iliyopatikana katika kipindi cha mwaka 1995 - 2002 ni kama ifuatavyo:-

(i) *European Union - USD 10m* (shilingi bilioni 10).

- Ukarabati wa miundo mbinu kama vile viwanja vya ndege na barabara, mfano uwanja wa ndege wa Mwanza na barabara ya Kigoma hadi Nyakanazi.
- Miradi ya kuboresha mazingira katika maeneo yote yaliyoathiriwa na Wakimbizi.
- Ukarabati wa zahanati nane katika Wilaya ya Ngara.
- Ukarabati wa Shule za Msingi katika Wilaya zinazoathirika na Wakimbizi.

(ii) *USAID* - Shilingi bilioni 2.

Msaada huu umeweza kusaidia katika:-

- Ukarabati wa barabara katika maeneo yalioathiriwa na Wakimbizi.
- Ukarabati wa mazingira kupitia Mradi wa Matumizi Bora ya Raslimali Mkoa wa Kagera *(Kagera Resource Management Project (KRMP).*

(iii) *WFP*

Msaada umeweza kusaidia katika:-

- Chakula tani 2000 kwa ajili ya wananchi walioathirika na Wakimbizi.

- Ukarabati wa barabara katika maeneo hayo.

(iv) *UNHCR - USD* bilioni 3.2

Msaada umeweza kusaidia katika:

- Kuboresha mazingira yaliyoathiriwa na Wakimbizi.

- Kuboresha utendaji wa Mikoa ya Kagera na Kigoma na Wilaya kwa kuwapatia vitendea kazi.

- Ukarabati wa Zahanati na shule katika maeneo yaliyoathiriwa na Wakimbizi.

(v) *IFAD - $ 16 million*

Msaada umeweza kusaidia katika:-

- Kusaidia sekta za kilimo, mazingira, mawasiliano, maji na afya katika Wilaya zenye Wakimbizi.

(vi) *UNDP/UNHCR - $ 3 million*

Msaada umeweza kusaidia katika:-

- Kuimarisha utendaji, uratibu na utoaji wa taarifa za miradi *(capacity building)* katika Wilaya zenye Wakimbizi.

(b) Mheshimiwa Spika, nchi rafiki za Tanzania zilizotoa misaada kwa Serikali yetu kusaidia athari katika maeneo ya Wakimbizi ni Canada, Japan, Denmark, UK, Netherlands, Switzerland, Belgium, France, Ireland na Germany.

(c) Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa kuhifadhi Wakimbizi imechangia kwa kutoa nyenzo mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Ardhi kwa ajili ya hifadhi ya Wakimbizi wapatao milioni moja.

- Viongozi kutumia muda wao mwingi katika kuratibu shughuli za Wakimbizi, gharama ambazo zingetumika kwa kuhimiza maendeleo ya wananchi wetu.

- Kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo kwa kupeleka askari wa ziada.

- Kutoa maeneo ya huduma za jamii kama shule, zahanati, viwanja vya michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia yaliyoelezwa hapo juu ni vigumu kupata gharama halisi kifedha ya nyenzo tulizochangia katika kuhudumia Wakimbizi. Aidha, Serikali inazishukuru nchi na Mashirika ya Kimataifa waliotoa na wanaoendelea kutoa misaada hii. Tunaomba wadumishe moyo huu hadi hapo tatizo la Wakimbizi litakapokwisha.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika Maziwa Makuu hivi sasa kumefanyika juhudi nyingi sana za kupata suluhu katika nchi ambazo zina migogoro na baadhi ya Wakimbizi wameanza kurudishwa makwao. Je, Serikali ina mpango gani zile *infrastructures* ambazo zipo kama mashule na barabara ya kuweza kuwahamishia raia wetu wakafaidika na zile huduma ambazo zipo katika Kambi zile?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba juhudi zinazoendelea za kuwapatanisha majirani zetu waliokuwa wanagombana jinsi amani inavyorejea katika nchi hizo ndivyo nao Wakimbizi sasa wanavyorudi.

Kwa mfano, sasa hivi Wakimbizi wote wa Rwanda wamesharejea kwao kwa sababu nchi yao ina amani na vile vile urejeshaji wa Wakimbizi wa Burundi unaendelea vizuri tangu vile vikundi ambavyo vilikuwa vinapigana baadhi kujiunga na Serikali.

Sasa yale maeneo ambako Wakimbizi walikuwepo wanapoondoka maeneo hayo tunakabidhi kwa Serikali za Mikoa na hasa kwenye Halmashauri husika ili wenyewe watazame namna nzuri ya kutumia maeneo hayo. Kwa mfano, katika Kambi walikuwa wanakaa Wanyarwanda kule Kitali baada ya kuifunga ile Kambi yale majengo tumekabidhi Halmashauri ya Biharamulo na tayari wameanza kuyatumia kama Sekondari na ndivyo tutakavyofanya katika maeneo yote ambapo Wakimbizi wakiondoka.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali moja la nyongeza. Tatizo la Wakimbizi na uzoefu tulioupata nao ni kwamba tumepata usumbufu sana hapa nchini ikiwa ni pamoja na kuharibu mazingira na pia kuvuruga usalama katika maeneo ambako kuna Wakimbizi na Mji wa Mwanza umeathirika sana kwenye jambo hili. Sasa swali ni kwamba, Wizara au Serikali imeweka msukumo gani kwa hawa ambao wanatusaidia ili watuongezee nguvu kwenye ulinzi na kutuliza hali irudi iwe salama kama tulivyokuwa hapo nyuma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sisi Tanzania kuhifadhi Wakimbizi tumepata athari mbalimbali na hasa katika ile mikoa ambayo wapo ya Kagera na Kigoma na Mikoa jirani kama Mwanza kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Sasa hivi katika kurekebisha hali hiyo bado tunazungumzia na wanaotusaidia ili waendeleze kutoa msaada kukarabati maeneo mbalimbali ambayo yemeharibiwa. Mwishoni mwa mwaka jana Wizara yangu imetiliana saini na Serikali ya Denmark wametoa shilingi 8 bilioni kwa ajili ya kurekebisha na kukarabati maeneo haya na wengine wengi watajitokeza. Maeneo yote pamoja na Mwanza. Nimesema katika kujibu swali la msingi wanafaidika vile vile na fedha hizi hata ukarabati wa ile *Airport* ya Mwanza umefanywa kwa fedha hizi. Kwa hiyo, Mwanza hatutaisahau.

Ameliliulizia suala la kuimarisha ulinzi. Tunashirikiana kati ya Wizara yangu na *UNHCR* kuweka ulinzi katika maeneo yote ya Wakimbizi na gharama za kuweka askari wale tunagawana kati ya Serikali ya Tanzania na *UNHCR* na mpango huu utaendelea mpaka Wakimbizi wote watakapoondoka.

Na. 117

**Ajira kwa Askari Wapya**

**MHE. MOHAMED ALI SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilikuwa na utaratibu wa kuajiri askari wapya kila baada ya kipindi fulani:-

(a) Je, katika kipindi cha 2003/2004 Serikali imeajiri askari wangapi nchini?

(b) Je, kwa upande wa Tanzania Zanzibar ni askari wangapi waliajiriwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Wingwi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka huu wa fedha (2003/2004), Bunge hili Tukufu liliidhinisha fedha za kuajiri askari Polisi 2,000. Maandalizi ya kuajiri askari hao yameanza na yanaendelea vizuri. Aidha, kupitia Bajeti ya mwaka jana (2002/2003) Jeshi la Polisi liliajiri askari wapya 1,679; miongoni mwao askari 337 walitoka Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali tunapenda kutoa shukrani kwa Bunge hili kwa hatua ya kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuajiri askari wapya kwa lengo la kuliongezea nguvu Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Ni utaratibu gani unaotumika katika kuajiri askari hasa Kisiwani Pemba hasa wakati huu wa mfumo wa vyama vingi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuajiri askari katika Jeshi la Polisi unafanana kwa Tanzania nzima amesema hasa kwa Pemba. Hatuna utaratibu tofauti na Pemba. *(Makofi)*

Kwa mfano mwaka huu hizi nafasi 2,000 utaratibu ni kwamba zinagawanywa katika Mikoa yote na Wilaya zote. Kila Wilaya au Mkoa unapata *ratio* yake ili tupate Jeshi lenye sura ya Kitaifa. *(Makofi)*

Sasa ni jukumu la kila Wilaya kutumia Kamati za Ulinzi na Usalama katika ngazi za Kijiji, Kata na Wilaya kuwachuja wale wanaoomba kwa sifa ambazo zimewekwa Kitaifa. Sasa kutokana na zile sifa ndipo tunapata wale askari wapya kila Wilaya inatuletea tunapeleka kozi wakishamaliza kozi wanaajiriwa na Jeshi la Polisi. Huo ndio utaratibu kwa nchi nzima pamoja na Pemba. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali imekuwa ikitoa uwezo mkubwa kwa Jeshi la Polisi ili kuhakikisha kwamba inapata askari wengi ambao wanaweza kulinda usalama wa nchi yetu. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuongeza vyuo vya kuzalisha askari wetu ambao wanaweza kutusaidia katika ulinzi wa nchi yetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baada ya ajira ya Polisi kusimamishwa miaka michache ya nyuma sasa Bunge hili mnatupatia fedha kwa ajili ya kila mwaka. Japo kusema kweli sisi tusingependa tuajiri wengi zaidi lakini uwezo wa kuajiri wengi zaidi unakuwa haupo. Kwa sababu hawa sasa hivi mnaotupatia ni kama tunafidia tu wale wanaostaafu, wale ambao wanaachishwa kazi kwa sababu mbalimbali na wale ambao wanafariki kwa magonjwa mbalimbali. Hata hivyo tunashukuru kwa hao mnaotupatia.

Sasa vyuo mpaka sasa tunavyo vyuo cha Polisi vitatu. Tuna chuo cha Polisi cha Moshi, Zanzibar na Kurasini - Dar es Salaam. Mpaka sasa vinafanya kazi vizuri hatujaelemewa kiasi cha kutaka tuongeze chuo kingine. Kwa hiyo, mbele ya safari kama hali ya uchumi itakuwa nzuri, kama tutapata sasa nafasi

kuajiri Polisi wengi zaidi pengine ndipo umuhimu wa kupata chuo kipya utakuja. Lakini kwa hivi sasa hivi vyuo vitatu vinakidhi mahitaji.

Na. 118

**Umeme Gologolo**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Kijiji cha Gologolo waliwahi kuahidiwa kupelekewa umeme na Waziri wa Nishati na Madini alipotembelea Kijiji hicho mapema mwaka 2001; na kwa kuwa licha tu kwamba Kijiji hicho kina viwanda vidogo vidogo vya mbao, kimeshirikishwa kusimamia shamba la miti na msitu wa asili wa eneo hilo; na kwa kuwa ziko ofisi kadhaa za Idara ya Misitu na pia Kijiji hicho kiko jirani sana na kituo cha usafirishaji kwa waya *(SKYLINE)* ambacho ni kivutio kikubwa sana kwa wageni:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa uamuzi wa kuupeleka umeme Gologolo kutoka Viti ulipo umeme sasa kiasi cha kilomita saba tu?

(b) Endapo Serikali iko tayari kupeleka umeme kijijini hapo, je, inatoa wito gani kwa wananchi ili wajiandae vizuri zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Jimbo la Mlalo, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali itafanya uamuzi wa kupeleka umeme Gologolo kupitia Shirika la Umeme *(TANESCO)* kutoka Kijiji cha Viti ulipo umeme endapo fedha zitapatikana. Ili kufikisha umeme katika Kijiji cha Gologolo Serikali inahitaji kiasi cha fedha za Kitanzania milioni 139.

(b) Serikali inatoa wito kwa wananchi kwamba kwa sasa fedha bado hazijapatikana lakini ili lisiwazuie hao kuendelea na ujenzi wa nyumba bora ili umeme ukifika Gologolo basi iwe ni suala la kuingiza umeme kwenye nyumba ambazo zinakidhi kuingiza umeme.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mafupi, lakini naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza nimfahamishe Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba nyumba bora anazozungumza tayari zipo na watu wanaendelea kujenga nyumba bora. Wanachoomba wananchi hawa ni Serikali itimize ahadi ya Waziri aliyekuwepo wakati huo kwamba umeme ufike pale Gologolo ambapo kuna taasisi mbalimbali na Ofisi za Serikali kama nilivyouliza katika swali la msingi.

Lakini la pili, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba alipata bahati ya kufika kwenye jimbo na maeneo ambayo tunayaombea umeme ufike. Sasa je, zile ahadi za Wizara hii kwamba umeme ufikishwe katika maeneo na vijiji mbalimbali kama vile Mlesa, Mlalo, Rangwi, Sunga, Mtahe na pale Mnazi sehemu ambayo Waziri alifika na kujionea. Je, jitihada hizo sasa ziko katika hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niseme kwamba ni kweli nimefika katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Mimi namshukuru yeye na wananchi wanaohusika kwa ukarimu wao wakati tukiwa kule.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi za Serikali kwenye maeneo husika. Ni kweli tulitoa ahadi kwamba tungeweza kuhakikisha kwamba umeme ufike katika maeneo husika pindi fedha zitakapopatikana.

Napenda niseme kwamba ilikuwa ni dhamira thabiti lakini katika kipindi cha hivi karibuni kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanafahamu Shirika la Umeme Nchini *(TANESCO)* limekumbwa na

uhaba mkubwa si kwa sababu kwamba hawafanyi makusanyo ya kutosha lakini makusanyo ya fedha zinazopatikana nyingi zinakwenda katika ununuzi wa mafuta kwa ajili ya kuzalisha umeme katika kipindi hiki cha ukame.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni gharama nyingi na matokeo yake ni kwamba baadhi ya miradi kwa kweli imebidi isimamishwe kutokana na umuhimu wa kuzalisha umeme kwa kiwango tulichokuwa nacho hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba endapo hali itakuwa nzuri basi zile ahadi ambazo zimewekwa zitatekelezwa na ahadi hutolewa kulingana na upatikanaji wa fedha sio kwamba ahadi zinatolewa tu kwa hali yoyote ile.

Na. 119

**Umeme wa Gridi - Mikoa ya Kusini**

**MHE. ABDULA S. LUTAVI** aliuliza:-

Kwa kuwa sote tunafahamu kwamba umeme ni suala la maendeleo na sio suala la anasa/starehe; na kwa kuwa Serikali imejitahidi sana kupeleka huduma ya umeme kwenye sehemu nyingi za nchi yetu.

Je, ni sababu zipi zilizoifanya Serikali ichelee kupeleka umeme wa Gridi katika Mikoa ya Kusini (Lindi, Mtwara na Ruvuma)?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Kuna njia nyingi ambazo zimependekezwa kutumika kupeleka umeme katika maeneo ya Mtwara, Lindi na Masasi kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa Gridi ya Taifa kwa njia ya laini ya kilovolti 220 kutoka Dar es Salaam hadi Mnazi Moja, Kituo cha kupoza umeme cha ukubwa wa 220/66/ na baadaye *33kv* katika maeneo ya Mnazi Mmoja na usambazaji wa umeme katika maeneo ya Mtwara, Lindi na Masasi. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi za Kitanzania bilioni 45.

(ii) Njia ya pili ambayo siku zote ilikuwa ikifikiriwa ni ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya Songo Songo katika maeneo ya Somanga wenye ukubwa wa 15 Megawati *(MW).* Laini ya kilovolti 132 kutoka Somanga hadi Mnazi Mmoja, Kituo cha kupoza umeme *(Sub-station)* katika maeneo ya Mnazi Mmoja pamoja na usambazaji wa umeme katika maeneo ya Mtwara, Lindi, Masasi. Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania bilioni 35.

(iii) Njia ya tatu ni ya kutumia gesi iliyopo eneo la *Mnazi Bay* inayodhaniwa kwamba ipo ambayo iko kwenye hatua ya awali ya kutathmiwa na Kampuni ya *Artumas Group Inc.* ya Canada. Kama nilivyosema siku chache hapa Bungeni mradi huu unagharimu shilingi bilioni 22.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuyapatia umeme maeneo ya Ruvuma, kuna njia mbili ambazo zimetathminiwa na baadhi ya njia hizo ambazo zimependekezwa na kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme *(Sub-station)* katika maeneo ya Makambako chenye ukubwa wa 220/66, laini ya kilovolti 66 kutoka Makambako hadi Songea. Pia kujenga kituo cha kupoza umeme *(Sub-station)* mjini Songea chenye ukubwa wa *66/33kV,* laini ya kilovolti 33 kutoka Songea hadi Mbinga pamoja na usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Ruvuma. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi za Kitanzania bilioni 47.

(ii) Mheshimiwa Spika, kuna wakati palifikiriwa pia utaratibu wa ujenzi wa Mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Nakatuta na kujenga laini ya kilovolti 66 kutoka Nakatuta hadi Songea, kituo cha kupoza umeme na pia kujenga laini ya umeme ya kilovolti 33 kutoka Songea hadi Mbinga pamoja na usambazaji umeme katika maeneo mengine ya Mkoa wa Ruvuma. Gharama ya mradi huu zinakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania bilioni 44.

Pamoja na mapendekezo hayo mbalimbali niliyoyataja hapo juu, pia kuna Mpango wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma. Mradi huu unatarajiwa kuyapatia umeme maeneo ya Mikoa ya Kusini yakiwemo maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo hapo juu ni wazi kuwa fedha zinazohitajika kupeleka umeme katika maeneo haya ni nyingi sana ukilinganisha na uwezo wa Serikali kwa sasa hivi. Ndiyo maana kutokana na tatizo la ukosefu wa fedha za kutekeleza miradi hii, Serikali imekuwa ikiendelea na juhudi zake za kuwasiliana na taasisi mbalimbali na wahisani mbalimbali ili kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana za kuweka mradi wa umeme wa kufikisha katika mikoa hii ya Kusini.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu haya ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa nifafanuliwe mambo mawili tu.

Inavyoonekana kwenye orodha hii ndefu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameitoa ya uwezekano wa kupata umeme kwa mikoa hii, inaonekana kama suala la gesi ndilo limefuatiliwa kwa karibu zaidi na gesi aliyoizungumzia kwamba iko kwenye hatua ambayo ni *advanced* kidogo ni ile ya *Mnazi Bay.* Sasa mimi nilitaka niulize hii gesi ya *Mnazi Bay* imekadiriwa kwamba ina uwingi wa kiasi gani unaoweza kutosha kwa mahitaji ya nishati hii muhimu kwa maeneo ya Lindi na Mtwara kwa muda gani kulingana na makadirio ambayo Serikali inayo kwa maeneo haya?

Mheshimiwa Spika, suala la pili nilikuwa nataka niseme inavyoelekea mpango wetu hasa sisi tunatakiwa tuweke utegemezi kwenye gesi kwa maana ya kupata umeme kwenye maeneo yetu yale. Kwa kulinganisha gesi ya *Mnazi Bay* na ile ya Songo Songo ni ipi ambayo inaweza kutuhakikishia sisi uendelevu wa uhakika wa upatikanaji wa nishati hii kwa maeneo yale ambayo tunayataja ya Lindi na Mtwara kwa mtazamo wa Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa makadirio ya awali gesi ya *Mnazi Bay* ingetosheleza kuzalisha umeme sio chini ya miaka 20 kwa kiwango cha umeme kisichopungua *megawatt 15* kwa mujibu wa mahitaji ya umeme ya maeneo husika ya sasa.

Lakini kama nilivyosema awali, masuala ya gesi kwa kuwa utafiti huu wa gesi ulifanyika katika miaka ya 1980 na muda mrefu umepita imebidi kualika tena wawekezaji kutafiti upya kiwango halisi cha sasa cha gesi ili kuweza kuhakikisha kwamba gesi iliyopo ni ya kiasi gani kwa sasa na gesi hii itaweza kuzalisha umeme kwa muda gani. Lakini natoa takwimu hizi kulingana na utafiti wa awali ambao ulifanywa kwa ajili ya gesi ya *Mnazi Bay.* Kama ambavyo nimesema siku chache zilizopita hapa Bungeni baina ya gesi ya Songo Songo na ya *Mnazi Bay.*

Kwa mujibu wa gharama ambazo nimezitaja hapa msukumo wa kwanza au kipaumbele cha kwanza kwa upande wetu kama itathibitika kama ambavyo tunatarajia itathibitika kwamba gesi ya *Mnazi Bay* ipo hivi katika kiwango kilichotathminiwa awali basi msukumo wa awali utakuwa katika kuzalisha umeme kupitia gesi ya *Mnazi Bay* kutokana na unafuu wa gharama kwa sasa.

Lakini pengine ningechukua nafasi hii kusema kwamba tunatarajia hawa wawekezaji wa *Mnazi Bay* ambao tumezungumza nao mara ya mwisho siku chache tu zilizopita sikutarajia kwamba watafika hapa nchini wiki ya kwanza ya mwezi Machi katika kuendeleza majadiliano ya mkataba wa ununuzi wa umeme *(Power Purchase Agreement )* na Serikali wako katika hatua za juu kabisa ambavyo nimewahi kusema hapa Bungeni na sasa hivi ni suala tu la kumaliza majadiliano hayo ili wao waweze kufanya mkusanyo wa fedha kwa ajili ya kutimiza mradi huu.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba tatizo kubwa ni uwezo wa Serikali kumaliza miradi hii; na kwa kuwa katika mkopo wa *Songas* shilingi bilioni 110, shilingi bilioni 64 zimebakia katika mradi ule; na kwa kuwa Mradi wa Songo Songo kupeleka umeme Lindi unagharimu shilingi bilioni 35, kwa nini Serikali haitaki kutumia hizo zilizobakia Songo Songo kupeleka umeme Kusini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli katika majadiliano ya utekelezaji wa mradi wa gesi ya Songo Songo kupitia *Songas,* ni kweli kwamba kuna kiasi fulani cha fedha ambacho kimebaki. Kutokana na umahiri wa majadiliano uliofanywa na wataalamu wetu na kuhakikisha kwamba gharama za awali za utekelezaji za mradi ule zinapungua, fedha hizi ambazo zimebaki zinatarajiwa pia kuingia katika mradi huo huo kwa sehemu kubwa ili kupunguza kiwango ambacho *TANESCO* wanatakiwa walipe kwa ajili ya ununuzi wa umeme huu yaani katika kulipia *capacity charge.* Bila ya kupunguza hivyo *capacity charge* ya mradi huu ungeweza ukawa mkubwa na ukawa ni mzigo kwa *TANESCO* na watumiaji wa umeme huu.

Kwa hiyo, kiasi fulani cha fedha kweli kipo lakini fedha hizi zinarudi katika kuhakikisha kwamba ule mpango mzima wa ununuzi wa umeme unafidiwa kiasi ambacho bei ya umeme kwa mtumiaji wa mwisho inakuwa ni ya unafuu zaidi hasa ikizingatiwa kwamba wakati ambapo gesi hii itakapoanza kutumika kwa kuzalisha umeme, *TANESCO* itatakiwa ilipe *capacity charge* kwa *IPTL,* itatakiwa ilipe *capacity charge* kwa mradi huu wa Songo Songo na kadhalika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Redio Tanzania wamezima matangazo yao sasa kwa sababu muda wa maswali umekwisha. Tunaendelea na mambo mengine. matangazo ya vikao vya leo vya Kamati mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anaomba niwatangazie Wajumbe kwamba wakutane kwenye chumba namba 219 leo saa 5.00 asubuhi. Kamati nyingine ni ya Kilimo na Ardhi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati wakutane leo Ijumaa tarehe 13 Februari, 2004 ukumbi namba 428 saa 5.00 asubuhi.

Kamati nyingine ya tatu na ya mwisho ni Kamati hii ya Fedha na Uchumi. Mwenyekiti anawakumbusha Wajumbe wa Kamati kuwa, leo tarehe 13 Februari, 2004 kutafanyika Kikao cha Kamati hiyo mara baada ya kipindi cha maswali na kikao kitafanyika chumba namba 133. Hivyo ndiyo vikao vya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwakumbusha juu ya semina zilizopangwa *weekend* hii. Tulipanga semina kesho Jumamosi ya *Rural Transportation.* Semina hiyo inaanza saa 3.00 asubuhi kama kawaida na Jumapili tulipanga vile vile semina nyingine ya Wakala wa Nishati Vijijini. Kwa kuwa ni Jumapili, tutaanza saa 5.00 asubuhi. Kwa hiyo, tuna semina mbili kesho na kesho kutwa. *(Makofi)*

Baada ya hapo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amewasilisha mezani leo *Supplementary Estimates* (Matumizi ya Ziada). Si mara nyingi tunafanya hivi, nadhani ni mara ya kwanza tangu Bunge hili limechaguliwa mwaka 2000. Kwa hiyo, nieleze utaratibu wake kwamba, masharti ya kanuni zote zinazohusu Makadirio ya mwaka ya Matumizi yaani ile Bajeti ya kawaida, masharti yote ya kanuni hizo yatatumika pia kwa matumizi ya nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, masharti yake ni kwamba, yanapelekwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi kuchambuliwa kwanza, halafu Mwenyekiti wa Kamati akishamjulisha Spika kwamba amemaliza kazi ya kuchambua inawekwa kwenye *Order Paper* ili ijadiliwe na Bunge.

Kwa utaratibu wa kawaida, Mheshimiwa Waziri anatoa maelezo halafu Mwenyekiti wa Kamati anatoa maoni ya Kamati. Pia, Mwenyekiti wa Upinzani anatoa maoni yake na baada ya mjadala huo tunaingia kwenye hatua ya pili ya *Supplementary Appropriation* yaani Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Makadirio haya kisheria sasa. Kwenye Bajeti ya kawaida huwa tuna *Appropriation Bill.* Hii ni

*Supplementary Appropriation Bill,* lakini itakuja baada ya kumaliza mjadala wa makadirio ya nyongeza yenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameomba niwajulishe kwamba, hakuna kodi mpya zinazoombwa kuidhinishwa na Bunge. Haya ni makato kutoka kwa mafungu yaliyopo ili kufidia gharama mpya ambazo zimejitokeza katika kipindi hiki.

Kwa hiyo, kazi yake pengine itakuwa ni nyepesi zaidi kuliko kama ingekuwa zinaombwa kodi mpya ziidhinishwe. *(Makofi)*

Mwisho wa matangazo tunaendelea na *Order Paper.*

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** *Speaker's guidance.*

**SPIKA:** *Okay, Speaker's guidance.* Leta Mheshimiwa Isaac Cheyo.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, jana tulipata hotuba nzuri kabisa ya Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge wote natumaini walifurahia *speech* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika *tradition* zako mara nyingi unatupatia muda wa kuweza kuizungumza kama Wabunge na kuchangia hoja ya Mheshimiwa Rais.

Je, unaonaje katika kipindi chako wakati utakapoona kwamba inafaa ukalipangia Bunge lako Tukufu kuzungumzia hoja ya Mheshimiwa Rais kama ilivyokuwa katika siku zako za nyuma? Ahsante. *(Makofi)*

*(Hapa Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge Walisimama Kuunga Mkono Kauli ya Mheshimiwa Isaac M. Cheyo)*

**SPIKA:** Hapana, hatoi hoja, anaomba *guidance* ya *Speaker* tu. Sasa *guidance* ni kama ifuatavyo: -

Nilisahau tu kutangaza jana kwamba, ni matakwa ya Kanuni zetu kwamba hotuba ya Rais inapangiwa muda wa kujadiliwa, ni matakwa ya Kanuni.

Kwa hiyo, nilighafirika tu jana sikusema hivyo, lakini tutaipangia muda wa kujadiliwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

## KAULI ZA MAWAZIRI

### UPEMBUZI YAKINIFU KUHUSU KUTOA MAJI YA ZIWA VICTORIA KWENDA MIKOA YA MWANZA NA SHINYANGA

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, wakati nilipokuwa nawasilisha Hotuba ya Makadirio ya Wizara yangu kuhusu Mipango na Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2003/2004, nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba mwezi Machi, 2003 Wizara yangu ilikuwa imekamilisha upembuzi yakinifu wa Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria kwa ajili ya Miji ya Kahama na Shinyanga na Vijiji litakapopita bomba kuu utakaogharimu jumla ya shilingi bilioni 85.5.4.

Madhumuni ya mradi huu ni kuwapatia maji wakazi wa Miji ya Kahama na Shinyanga pamoja na Vijiji 54 vya Mikoa ya Shinyanga na Mwanza ambavyo bomba la maji litapita. Vijiji husika viko katika Kata 13 kama ifuatavyo: -

Kata za Oljimate, Lubili, Mwamile katika Wilaya ya Misungwi Mkoani Mwanza. Kata za Salawe, Solwa, Iselemagazi, Mwantini, Pandagachiza na Nyabukunde Wilaya ya Shinyanga Vijijini na Kata za

Kinaga, Bulige na Ngaya katika Wilaya ya Kahama. Mradi huu umefanikiwa kukidhi mahitaji ya maji kwa wakazi 420,000 kwa sasa na baadaye watu 940,000 katika upeo wa miaka 20 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, tarehe 03 Februari, 2004 hapa Dodoma, Serikali ilitiliana saini mkataba na Mkandarasi *MS China Civil Engineering Cooperation Company* ambaye atajenga awamu ya kwanza ya mradi huu. Sherehe hii ilihudhuriwa pia na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mikoa ya Ziwa. Awamu hii itahusisha ujenzi wa chanzo cha maji, chujio la maji, mitambo ya kusukuma maji, bomba kuu la maji na tanki kuu kwenye mlima wa Mabale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusainiwa mkataba huu kumekuwepo na upotoshaji wa jambo hili katika baadhi ya Vyombo vya Habari vya ndani na nje ya nchi hasa suala la mkataba uliowekwa na Serikali ya Misri na Sudan na Watawala wa Kikoloni wa Tanganyika wakati ule na matumizi ya maji haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe historia fupi. Mwaka 1929 Serikali ya Ukoloni ya Tanganyika kwa wakati huo ilitiliana mkataba na Serikali za Misri na Sudan kwamba nchi yetu haiwezi kutumia maji ya Ziwa Victoria bila kibali cha nchi hizo.

Mwaka 1952 Mkataba huu ulihuishwa tena. Lakini tunamshukuru sana Baba wa Taifa letu, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwamba, baada ya Uhuru mwaka 1962 alieleza kwenye Umoja wa Mataifa kuwa, Serikali ya Tanganyika wakati ule haitambui Mkataba huo na alisisitiza kwamba Serikali itaendelea kufanya mazungumzo na watumiaji wa maji wa Bonde la Mto Nile kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba pande zote zinanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu bado ndiyo msimamo rasmi wa Serikali yetu kuhusu mkataba huo. Ninafurahi kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba, miaka hii yote kumekuwa na mazungumzo na nchi ambazo zinatumia maji ya Ziwa Victoria. Kwa mfano, Desemba, 2003 kulikuwa na mkutano Addis Ababa - Ethiopia, wa Mawaziri wa Maji wa Nchi 10 zinazotumia Maji ya Ziwa Victoria na kukubaliana kwamba kila nchi itateua Wataalam watatu wakiwemo Wanasheria ili kutengeneza Mkataba wa Makubaliano wa Matumizi ya Maji ya Ziwa Victoria. Kazi hii bado inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkataba ule ulisisitiza zaidi matumizi ya umwagiliaji. Ningependa kuweka bayana kuwa maji tunayoyachukua chini ya mradi huu kutoka Ziwa Victoria ni kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo tu na siyo vinginevyo.

Ninarudia, maji tunayoyachukua chini ya mradi huu kutoka Ziwa Victoria ni kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo tu na siyo vinginevyo. Isitoshe, chini ya mradi huu tunachukua lita 1,250 tu kwa sekunde kutoka ziwani ambazo ni kidogo sana na hivyo hakutaathiri maslahi ya watumiaji wengine wa maji katika Bonde la Mto Nile. Tungependa kila mtu na hasa watumiaji wenzetu katika Bonde la Mto Nile watuelewe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa kulisukuma na kulifuatilia jambo hili. Sasa, napenda kutoa wito kwao, kwa viongozi wengine na wananchi wa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga kupokea mradi huu ambao wameuomba kwa miaka mingi na kuhakikisha kwamba wanashiriki kikamilifu katika hatua zote zilizobaki katika mradi na hatimaye utakapokamilika waumiliki na kuuendesha kwa njia endelevu inayotekeleza Sera ya Maji ya mwaka 2002. Ningependa kuwahakikishia kwamba, sisi Wizarani tutafanya kila tuwezalo ili mradi huu ukamilike kabla Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, hajaondoka madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hizo ndiyo kazi peke yake tulizozipanga kwa ajili ya kikao cha leo. Hii ni kwa sababu Shughuli za Serikali zote zimekamilika kwa maana ya Miswada na Maazimio. Shughuli ya Serikali peke yake iliyobaki ni Makadirio ya Nyongeza, nitayapeleka sasa hivi kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ili wayashughulikie.

Kwa hiyo, matumaini yetu ni kwamba, tutaweza kuiweka hii kwenye *Order Paper* ya Jumatatu, halafu baada ya hapo kwenye *Order Paper* tutakuwa tunaweka Taarifa za Kamati zetu za Kudumu (taarifa za mwaka jana) ili tuweze kuzipokea na kuzijadili kama itaonekana kuna haja ya kuzijadili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo basi, kwa kuwa hatuna shughuli nyingine ya Serikali wiki hii, sasa naahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 04:40 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 16 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*